HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO

Shule ya Sekondari Soitsambu,

MKOA WA ARUSHA
SIMU No. +255769180300

Kumb Na……

S.L.P 56

LOLIONDO.

Tarehe 12/12/2022

MZAZI/MLEZI WA……..

Shule ya Msingi……..

S.L. P……

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI SOITSAMBU WILAYA YA NGORONGORO MKOA WA ARUSHA MWAKA 2023

1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Soitsambu kwa mwaka 2023. Shule ya sekondari Soitsambu ipo umbali wa kilomita 25 magharibi mwa makao makuu ya halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro.

Usafiri wa basi kutoka mjini Loliondo unapatikana katika kituo cha mabasi cha Wasso. Nauli ni Tsh. 5,000/=

Muhula wa kuanza wa masomo unaanza tarehe 09/01/2023 unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 08/01/2023 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 15/01/2023.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

2.1 SARE ZA SHULE

a) Wavulana;

- suruali ya kitambaa rangi ya dark blue 2

-shati nyeupe mikono mifupi 2

-sweta rangi ya dark blue 2

-viatu vyeusi vya Kamba visivyo na visigino virefu, mabuti au raba.

-Soksi nyeusi pea 2

-Tarck suit dark blue yenye nembo ya shule 25,000/

Edit with WPS Office

- Tshirt yenye nembo ya shule tsh 12,000/=

-Tai ya mistari ya rangi ya dark blue na nyeupe

NB mtindo wa mnyonyo kwa wavulana haukubaliki shuleni

b. wasichana

-Sketi ya rangi dark blue, ndefu inayofika kwenye soksi yenye mshono wa V kwa mbele na isiyo bana mwili.

- shati nyeupe mikono mifupi 2.

-sweta rangi ya dark blue 2.

-Soksi nyeupe 2

-viatu vyeusi vya kamba visivyo na visigino virefu na visiwe raba.

-Trck suit dark blue.

- Tshirt yenye nembo ya shule tsh 12,000/=

- Rangi ya Hijab iwe nyeupe na isio na urembo wowote

NB; Sketi za kubana kwa wasichana au zisizovuka magoti hazikubaliki kabisa.

SHAMBA DRESS; - sketi 2 za kitambaa cha kaki zenye mshono wa kawaida kwa wasichana

- suruali 2 kwa wavulana za kitambaa cha kaki zenye mshono wa kawaida

SARE YA MICHEZO;

- bukta rangi ya light blue/blue bahari 2
- tshirt rangi ya light blue/blue bahari 2
- raba za michezo 2
- soksi ndefu rangi ya blue 2

VIFAA VINGINE MUHIMU

-Chandarua 1 kwa ajili ya kujikinga na mbu.

-Rangi ya viatu, kiatu cha ngozi nyeusi kisicho na kisigino kirefu vyenye kamba kwa wasichana na wavulana .

-Nguo za ndani pea 2 au zaidi kwa wavulana na wasichana

-Taulo za kike (pedi) packets 2 au zaidi kwa wasichana .

Edit with WPS Office

- Daftari 10 (Counter books quire 3 au 4), file, penseli, kalamu na mkebe wa hesabu

-Ream moja ya A4 kwa ajili ya kufanyia mitihani na mazoezi kwa matumizi binafsi ya mwanafunzi kwa mwaka wa masomo.

- Pia unashauriwa kumnunulia mwanao vitabu binafsi vya kujisomea vya masomo yote tisa vilivyoandikwa na oxford au Taasisi ya elimu Tanzania (TIE) kwani muhimu sana kitaaluma kwa mwanafunzi

-Nauli ya wanafunzi kwenda shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo,

- Godoro inchi 2.5 (mbili na nusu) 1

-Blanketi 1

- Ndoo ya plastic lita 10

- Vyombo vya kulia chakula vyote vya bati

sahani,

kikombe,

bakuli na

kijiko.

- Taulo la kuogea/khanga kwa wasichana

- Shuka za blue iliokolea kwa wavulana na rangi ya pinki iliokolea kwa wasichana pea 2

- Dictionary oxford 7th **edition** ya kiingereza kwa kiingereza 1

VIFAA VYA USAFI WA MAZINGIRA; - slesha, mopa ,fagio la chelewa n.k.

Zingatia;-Kila mwanafunzi aletwe shuleni na mzazi wake

- Kila mzazi amkatie mwanae bima ya afya (CHF) ili aweze kupata huduma za matibabu endapo atazihitaji akiwa shuleni.

3.0 Sheria na kanuni muhimu za Shule hii.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa sheria namba 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu sayansi na teknolojia yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Rais–TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote , wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

Edit with WPS Office

b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.

c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (night preparation)

d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule

g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa

h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote, na

i) Kutunza mali za umma.

4. Makosa Yafuatayo Yanaweza Kusababisha Kufukuzwa au Kusimamishwa shule

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli, sigara, ugoro na kadhalika.
e) Kupigana au kupiga

f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma au miundombinu ya shule.

g) Kudharau Bendera ya Taifa

h) Kuwa mjamzito/ /kusababisha mimba

i) Kuoa au kuolewa

j) Kutoa mimba

k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

l) Kukataa adhabu kwa makusudi

m) Kuwa na simu ya mkononi.

n) Utoro wa zaidi ya siku tisini (90).

Edit with WPS Office

4.0 Mambo Mengine Muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi.

a) Medical Examination Form inatakiwa kujazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.

b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wakutoshiriki katika migomo , fujo, na makosa ya jinai.

c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

5.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo /maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

……

ALEX B. MASSAWE

MKUU WA SHULE

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART A

To The Medical Officer

.....

.....

Mr. & Mrs. /Miss.....

Please examine the above name as to his/her fitness mentally and for a full time secondary Education. The examination should include the following categories (i-iii) each category or sub-category of which will render the applicant ineligible in case of any defects.

Pregnancy (category IV) will also render a girl candidate in eligible for the secondary Education.

i. (a) Eye-sight
   (b) Hearing
   (c) Limbs
   (d) Speech
   (e) Venereal Diseases
   (f) Leprosy
   (g) Epilepsy
ii. Neuroses
iii. Other serious diseases
iv. Pregnancy

DATE.....SIGANATURE.....

PART B

I have examined the above named and consider that he/she is fit/unfit for full time Secondary Education.

i.

Edit with WPS Office

a) Eye-sight.....
b) Hearing.....
c) Limbs.....
d) Speech.....
e) Venereal Diseases.....
f) Leprosy.....
g) Epilepsy.....
ii. Neuroses.....
iii. Other serious diseases.....
iv. Pregnancy.....

DATE.....SIGNATURE.....DESIGNATION.....

Edit with WPS Office